

MWISHO WA KIPINDI CHA DHARURA YA AFYA
YA UMMA KUTOKANA NA COVID-19


Mabadiliko ya Manufaa ya Afya COVID-19

Mnamo **tarehe 11 Mei 2023**, muda wa dharura ya afya ya umma utaisha. Dharura za afya ya umma huruhusu serikali kutumia pesa haraka na kubuni mipango mipya ili kusaidia afya ya umma.

Hata kama muda wa dharura ya afya ya umma utaisha, bado COVID-19 ni ugonjwa hatari.



- ✓ Bado watu wengi wanakufa kila siku nchini Marekani, na wengine wengi wanaugua zaidi.
- COVID-19 inaweza pia kukatiza ratiba zako na za familia yako, na kuwazuia watu kwenda kazini au shuleni.



Huenda ukatakiwa kulipia vipimo, matibabu na chanjo za COVID-19.

Katika kipindi cha Dharura ya Afya ya Umma, chanjo, matibabu na vipimo vya COVID-19 havikulipishwa. Baada ya tarehe 11 Mei, gharama ya matibabu, vipimo na chanjo itategemea bima yako ya afya.



Iwapo una Medicaid, utahitaji kuthibitisha kuwa unastahiki kupokea huduma kila mwaka.

Katika kipindi cha Dharura ya Afya ya Umma, watu waliokuwa na bima ya afya kupitia Medicaid waliandikishwa kiotomatiki kila mwaka. Baada ya tarehe 31 Machi, watu watahitaji kuthibitisha kuwa wanastahiki kupokea huduma kila mwaka.



Ukiwa unatumia SNAP, huenda ukapokea pesa kidogo za chakula kutoka kwa serikali.

Katika Kipindi cha Dharura ya Afya ya Umma, serikali ilizipa familia ambazo hutumia Mpango wa Usaidizi wa Lishe ya Ziada (SNAP) pesa za ziada za chakula. Hivi karibuni familia zitaacha kupokea pesa hizi za ziada.

**PATA CHANJO NA VIPIMO LEO
WAKATI BADO HAVILIPISHWI.**



NRC-RIM

National Resource Center for
Refugees, Immigrants, and Migrants

Zifuatazo ni hatua ambazo unaweza kuchukua kabla na baada ya PHE kuisha ili kujilinda na kulinda jamii yako.

Iwapo una Medicaid:

- Hakikisha kuwa shirika linalodhibiti manufaa yako ya Medicaid lina maelezo yako ya mawasiliano, ikiwa ni pamoja na anwani na nambari yako ya simu.
- Soma kwa makini zaidi barua pepe unazopokea zinazohusiana na manufaa yako ya Medicaid. Ukipokea ilani, ichukulie hatua mara moja.

Pata dozi zote za chanjo za COVID-19 wakati bado hazilipishwi.

- Kupata chanjo zote inamaanisha kupata dozi zote mbili za chanjo inayotolewa mara mbili, na kupata dozi zozote za ziada zinazopendekezwa.
- Iwapo hujapata chanjo zote, kuna uwezekano mkubwa wa kuambukizwa COVID-19, kuwa mgonjwa sana au kufa.
- Ni muhimu kupata dozi zote za chanjo ya COVID-19, hata baada ya tarehe 11 Mei. Tafuta kliniki za afya ya jamii na maeneo mengine yanayotoa huduma za afya bila malipo au kwa bei nafuu.
- Tafuta chanjo katika [vaccines.gov](https://www.vaccines.gov).

Pata vipimo vya nyumbani vya COVID-19 kabla ya tarehe 11 Mei.

- Agiza vipimo visivyolipishwa vya COVID-19 kutoka kwa serikali kabla ya tarehe 11 Mei. Vipimo vinne kwa kila nyumba vinaweza kuagizwa bila malipo kila mwezi. Agiza vipimo mtandaoni katika [covidtests.gov](https://www.covidtests.gov), au upige simu kwa 1-800-232-0233 ili uagize vipimo, katika zaidi ya lugha 150.
- Iwapo una bima ya afya, ikiwa ni pamoja na Medicaid, unaweza kupata vipimo visivyolipishwa vya COVID-19 kwenye maduka mengi ya dawa hadi tarehe 11 Mei. Nenda kwa duka la dawa lililo karibu, wape kadi yako ya bima, na uwaulize iwapo vipimo vya COVID-19 vinalipiwa na mpango wako wa bima.

Kuna chaguo nyingi kwa watu wanaohitaji usaidizi wa kulipia chakula.

- Wasiliana na hifadhi yako ya karibu ya chakula kwa kutembelea [foodfinder.us](https://www.foodfinder.us) na kuweka msimbo wako wa eneo.
- Baadhi ya majimbo yana mipango inayokuruhusu kununua matunda na vyakula zaidi kupitia manufaa yako ya SNAP. Tembelea [doubleupamerica.org](https://www.doubleupamerica.org) ili upate maelezo zaidi.
- Uliza kama kuna vyakula visivyolipishwa na vinavyotolewa kwa bei nafuu katika shule ya mtoto wako.
- Piga simu kwa 2-1-1, au 1-866-3-HUNGRY, au umwulize msimamizi wako wa makazi kuhusu rasilimali nyingine za chakula.



Tafuta Chanjo



Agiza Vipimo



Tafuta Hifadhi ya Chakula



Ukipata ugonjwa wa COVID-19 baada ya tarehe 11 Mei, usichelewe kupokea matibabu. Hata kama utahitaji kulipia dawa, gharama zako za afya zitakuwa juu zaidi ukisubiri kwa muda mrefu na utahitaji kulazwa hospitalini.